**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALIMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BIBI TITI MOHAMED**

**MKUU WA SHULE: +255 714 928 760**

**MAKAMU MKUU WA SHULE: + 255 621 979 891 / +255 767 921 725**

**E-mail: bibititimohamedisecondaryschoo@gmail.com**

---

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI …………………………………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BIBI TITI MOHAMED MWAKA 2026**

**01.** Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga Kidato cha kwanza mwaka 2026 katika shule ya Sekondari ya wasichana **BIBI TITI MOHAMED**. Tunampongeza kwa mafanikio hayo. Shule ya Sekondari ya wasichana BIBI TITI MOHAMED ipo katika **Mkoa wa Pwani**, **Halmashauri ya Mji Rufiji umbali wa kilomita 196 Kutoka Dar- es- salaam**. Inapatikana **Mji mdogo wa Utete**, **Kitongoji cha Kindwitwi**. Kwa Mwanafunzi anayetoka Mikoa ya kusini (Lindi na Mtwara) ashuke Ikwiriri, na Mwanafunzi anayetoka Mikoa mingine afike **Dar - Es – Salaam -Mbagala Rangi Tatu** stendi ya magari ya kuelekea kusini mwa Tanzania ndipo atapata magari ya moja kwa moja kuelekea **Utete** na **atateremka Shuleni BIBI TITI MOHAMED**.
Muhula wa Masomo utaanza tarehe **13/01/2026**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni siku ya **jumanne ya tarehe 13/01/2026**. Mwanao atapokelewa Shuleni endapo atasoma vyema maelekezo na kukubaliana nayo na kutimiza mambo yaliyomo.

**MUHIMU**: Ni matumaini yetu kwamba mwanao atasoma na kuzingatia maelekezo yote na Mzazi/Mlezi utamtimizia mahitaji yote kabla ya kuripoti shuleni ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.Kama kuna changamoto au maswali yoyote unaweza kupiga simu kwa namba zilizoainishwa hapo juu.

## 02. Mambo muhimu ya kuzingatia

### 2.1 Sare za shule

- **(i)** T-shirt moja **RANGI YA MAROON**
- (ii) T shirt moja **Nyeupe ya TAIFA STARS** kwa ajili ya michezo
- (iii) Sketi mbili rangi ya DRAFT imeambatanishwa kwenye fomu hii. Zote ziwe zenye urefu kuvuka magoti MSHONO WA RINDA BOX. Unaweza kushona nyumbani sketi moja na nyinine inapatikana shuleni.
- (iv) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vya kufunika visiwe na visigino virefu (Jozi 2)
- (v) Shati nyeupe mbili mikono mifupi /nusu kanzu mbili na hijabu yake kwa wanaotaka (kitambaa cha harua)
- (vi) Soksi rangi nyeupe jozi 2 au Zaidi
- (vii) Viatu vya michezo na kushindia (raba rangi nyeupe) na SANDAL ZISIZO NA UREMBO.
- (viii) Kandambili kwa ajili ya kuogea tu
- (ix) Hijabu rangi Nyeupe kwa ajili ya kushindia kwa wanaovaa Hijabu isiyo na urembo
- (x) Sweta moja rangi ya maruni (maroon)
- (xi) Kila mwanafunzi lazima aje na Tracksui za **GREY** kwa ajili ya michezo na kujisomea wakati wa usiku.
- **(xii) Gauni la Solo kitambaa cha Tetron chenye Draft Ndogo ndogo za Blue na Nyeupe kwa ajili ya kushindia. Unaweza kushona shuleni au nyumbani.**

**ZINGATIA**: *Mavazi ya nyumbani hayaruhusiwi kabisa shuleni. Mwanafunzi anapaswa kuripoti akiwa amevaa tracksuit.*

### 2.2 Mahitaji mengine ya Bweni

Mwanafunzi anapaswa kuja na mahitaji yafuatayo;

- (i) Godoro la nchi 4 urefu wa futi mbili na nusu kwa sita lenye kava ngumu isiyovujisha maji. Unaweza kulinunua kwenye duka la shule .
- (ii) Shuka rangi ya pink tatu (03)
- (iii) Mto na foronya 2 za pinki
- (iv) Taulo
- (v) Nguo za ndani/chupi Zaidi ya 12 NA TAULO ZA KIKE paketi sita.
- (vi) Ndoo tatu zenye mifuniko lita 10 (ndoo 2 kwa matumizi ya mwanafunzi na ndoo 1 kwa matumizi ya jikoni)
- (vii) Sanduku imara la bati moja lenye makufuli mawili (tranker)
- (viii) Vyombo vya chakula, chombo chenye mfuniko alimaarufu kama CONTENA, Kijiko, Chupa ya chai ndogo.
- (ix) Chandarua futi 3 x 6 pembe nne.
- (xiii) MWAMVULI mmoja mdogo, TOCHI au TAA YA SOLAR kwa ajili ya kujisomea umeme unapokata
- (xiv) Mfuko maarufu unaoitwa SHANGAZI KAJA kwa ajili ya kuhifadhia madaftari.

### 2.3 Mahitaji ya Taaluma darasani

- (i) Rimu 2 kwa mwaka size A4
- (ii) Cheti cha kuzaliwa halisi na Nakala
- (iii) Madaftari 12 (Counter Book), Kalamu Peni/Penseli za kutosha
- (iv) Mathematical Sets na English Dictionary.
- (v) Faili 2 kwa ajili ya kuhifazia mitihani na kumbukumbu zingine ‘FILE FOLDER’
- (vi) Graph pad (Graph papers)
- (vii) Begi la kubebea madaftari.
- (viii) Vitabu vya TIE vya form one kwa masomo yote vya mtaala ulioboreshwa

**2.4 Mahitaji mengine**

(i) Fagio laini (softbloom)
(ii) Fagio la chelewa la wima lenye mpini (kufagilia nje)
(iii) Rubber squizer
(iv) DUSTBIN KUBWA

PIA, Shule yetu ina eneo kubwa la kilimo hivyo mwanafunzi aje na vitu vifuatavyo

(i) Jembe
(ii) Fyekeo
(iii) Reki imara

**ZINGATIA**: Kwa **kupunguza gharama na usumbufu wakati wa safari baadhi ya vifaa unaweza kuvinunua katika duka la shule. NA**

**KILA MWANAFUNZI AKUMBUKE KUJA NA BIMA YA AFYA KWA AJILI YA KURAHISISHA GHARAMA ZA MATIBABU PINDI AWAPO HAPA SHULENI, KAMA HANA AFIKE NA FEDHA ZA KITANZANIA SHILINGI 50,400/= KWA AJILI YA KULIPIA BIMA YA NHIF.**

**03. Sheria na kanuni muhimu za shule**.

Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII, USAFI na TABIA NJEMA kwa ujumla Wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia kauli na vitendo hivyo:

(a) Mwanafunzi atasimama anapomsalimu mwalimu, mtumishi wa shule au mtu yeyote aliyemzidi umri

(b) Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu na ya kihuni popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.

(c) Hairuhusiwi Kwa mwanafunzi

(i) Kufuga kucha na kusuka nywele hairuhusiwi

(ii) Kunyoa kipara

(iii) Kutia dawa nywele (curly) na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa

(iv) Kuvaa vitu kama mapambo mfano Hereni, Mikufu bangili au vitu vya kiimani kama vile Rozali, Kofia, Kanzu, kwa kuwa Shule hii ni ya Serikali. Kuwa na mafuta au manukato yenye harufu kali.

(v) Kuvaa kandambili kwenye Bwalo la chakula na Ofisi zote za shule

(vi ) Kuvaa sketi chini ya kiuno au Kuvaa nguo za mtindo, mfano- model

(d) Mwanafunzi atasimama kwenye mstari wakati wa kupata huduma

(e) Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza au kujibu swali

(f) Anatakiwa kuwa mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyo sababisha usumbufu kwa wengine anapokuwa Darasani Maktaba, bwenini, wakati wa kujisomea (prepo) na katika mikusanyiko yoyote mfano paredi nk

(g) Mwanafunzi LAZIMA awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule.

Hivyo Mwanafunzi:

(i) Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.

(ii)Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa

(iii) Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa

(iv) Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki wa uwepo wake shuleni (Roll call). Ukaguzi wa Usafi,

kupandisha Bendera ya Taifa na Mikutano ya darasa .

(v))Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria maandalio ya Alasiri (9;30-10:30) na usiku kuanzia saa 1;00 - 5;00 .kwa siku ya Jumamosi maandalio ya masomo yataanza saa 4 asubuhi hadi saa 7 mchana

(h) NI LAZIMA mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na KITAMBULISHO kwa nyakati zote awapo

shuleni na nje ya shule.

(i) Jumapili ya Mwisho wa mwezi ni siku ya wanafunzi kwenda kupata mahitaji yake muhimu kuanzia

6 mchana hadi saa 8 Mchana. Zingatia muda na haupaswi kwenda sehemu nyingine yeyote bila ruhusa.

(j) NI LAZIMA mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje

ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu, anapaswa kuwa na kibali (GATE PASS) cha

maandishi.(Kilichotolewa na Mkuu wa shule au Mwalimu wa Zamu)

(k) Mwanafunzi haruhusiwi kujipikia chakula bwenini, wala kutumia electrical heater au jiko la aina yoyote pia **PASI YA UMEME HAIRUHUSIWI** aje na **PASI YA MKAA**.

(l) Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni pasipo kibali cha Mkuu wa Shule na ikiwa kibali kimetolewa kikundi au chama kitatakiwa kuandika muhutasari wa kikao na nakala kuwasilishwa kwa Mkuu wa Shule.

(m). USAFI: Mwanafunzi anawajibika kuwa msafi kwa mavazi na mwili wake na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi.

(o) Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare za shule muda wote akiwa ndani na nje ya shule na achomekee shati au T shirt yake. Mavazi ya nyumbani Hayaruhusiwi kabisa.

(p) Hairuhusiwi mwanafunzi kumiliki simu au sehemu ya simu kama laini, Charger, earphone, Ipadi smart watch nk.

(q) Hairuhusiwi kujihusisha na mikutano ya siasa katika kipindi chote awapo mwanafunzi.

(r) MAENEO YASIYORUHUSIWA: Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo bila sababu maalumu, **Ofisi za shule , Chumba cha wafanyakazi ,Maabara , Jikoni, Nyumba za wafanyakazi ,Vilabu vya pombe ,Majumba ya starehe , Majumba ya kufikia wageni.**

(s) BWENINI Kila mwanafunzi atawajibika kufanya usafi wa kila siku katika eneo atakalopangiwa na kiongozi wake pia mwanafunzi haruhusiwi kumkaribisha mgeni yeyote bwenini wakati wowote, na ni marufuku kupeleka viti , meza na chakula Bwenini.

(t)Mwanafunzi hatakiwi kuja na chakula cha aina yoyote kutoka nyumbani.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi**

- **Mwanafunzi awapo shuleni anatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kinatumika na mwanafunzi mmoja tu.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi kwa ruhusa na kibali maalumu kutoka kwa Mkuu wa Shule.( Msiba au Ugonjwa)**

**04. MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI AU KUSIMAMISHWA SHULE:**

1. Wizi

2. Uasherati, ushoga na ulawiti.

3. Ulevi wa aina yoyote

4. Utumiaji wa madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa sigara, Shisha, Bangi,Cocaine ,Mirungi,Kubeli nk.

6. Makosa ya jinai

7. Kuoa au kuolewa

8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

9. Kupigana au kumpiga mwingine.

10. Kudharau Bendera ya Taifa

11. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule

12. Kuchochea au kufanya vurugu, kugoma Kwa namna yoyote

13. Kutoa lugha ya matusi

14. Kumdharau kiongozi wa shule, mwalimu, mfanyakazi na jamii kwa ujumla

15. Kutohudhuria vipindi, kufeli majaribio na mitihani ya mara kwa mara shuleni.

17. Kuwa na simu ya mkononi.

18. Kuwa mchafu kupindukia katika mwili, mavazi na mazingira yanayokuzunguka.

19. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi za kuchana na kitana kidogo ni marufuku kunyoa kiduku, wave, kusuka au kusokota dredi, au rasta na kuvaa wigi

**05. Viambatisho na Fomu**

a. fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.
b. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makossa ya jinai
c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule na
d. Picha nne (04) za wazazi/walezi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za simu

**06. Tafadhari soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa shule …………………………….....**

**Jina la mkuu wa shule: CHIKU JUMANNE MHANDO**

**Mhuri wa mkuu wa shule: …………………………………..**

**PRIME MINISTER OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**BIBI TITI MOHAMED GIRLS SECONDARY SCHOOL**

**P.O.Box. 45**

**UTETE- RUFIJI**

**Date: …………………......**

**To:**

**THE MEDICAL OFFICER.**

…………………………….

…………………………….

Please examine………………………………………………………………………………………

As to her fitness for pusuing further education at this school

- Hemoglobin ……………………………………………………………………………….
- P.V. Blooding ………………………………………………………………………………
- (A) Blooding ……………………………………………………………………………….
- (B) Hearing …………………………………………………………………………………
- Blood pressure ……………………………………………………………………………..
- Urine for Sugar and Pregnancy tests ……………………………………………………….
- Stool for routine examination ……………………………………………………………….
- Asthma ……………………………………………………………………………………..
- Skin diseases ……………………………………………………………………………….
- Leprosy ……………………………………………………………………………………..
- Pulmonary tuberculosis ……………………………………………………………………..
- Employs …………………………………………………………………………………….
- Deformity …………………………………………………………………………………...
- Mental problem ……………………………………………………………………………

Comment ………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
…………

**Date:** …………………………………… **DESIGNATION** ……………………………………………….

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**HALMASHAURI YA MJI RUFIJI**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BIBI TITI MOHAMED**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI**

**A. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI (ijazwe na Mwanafunzi mwenywe)**

Jina kamili kamili( kama alivyosajiliwa darasa la saba) …………………………………………………………….

Tarehe ya kuzaliwa ………………. kabila …………….. Dini na dhehebu ……………………………………………

Shule nitokayo ……………………………….. mahali ninapoishi …………………………………………………

Mkoa …………………………………………… Anuani …………………………………………………….

Jina la baba/mlezi …………………………………………….. kazi yake ……………………………………………

Jina la mama/mlezi ……………………………………………. Kazi yake ……………………………………………

Wazazi/walezi wanaishi (wapi) ………………………………… pamoja /au wametengana ………………………….

Anuani ya mzazi/mlezi ……………………………………….. Simu ………………………………………………….

Wakati wa likizo nitakuwa kwa ( mtaje) …………………………………………….. wapi ………………………….

Nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli na sahihi;

Sahihi ya mwanafunzi ………………………………….. tarehe …………………………………………………….

KUKUBALI (mwanafunzi mwenyewe ajaze)

Mimi ………………………………………………………….. nimesoma maagizo kwa makini na kuzielewa taratibu za shule na nipo tayari kuzifuata, Hivyo ninakubali nafasi niliyopewa na nitafika shuleni tarehe iliyopangwa.

**B. IJAZWE NA MZAZI AU MLEZI**

Mimi …………………………………………………. ambaye ni …………………………………..wa mwanafunzi huyu nimesoma kwa makini maelekezo pamoja na sharia za shule katika fomu ya kujiunga. Nipo tayari ajiunge na shule hii, naahidi kumpa mahitaji yote ili aweze kupata elimu yake vizuri katika shule hii. Aidha nitasaidiana na walezi wa shuleni katika kumlea mwanafunzi huyu katika maadili mema na kuitikia wito wa kufika shuleni pale nitakapohitajika

Anuani yangu ya kudumu ……………………………………. Simu ………………………………………….

Nikipata uhamisho ama kubadilisha makazi nitaijulisha shule kwa maandishi.

Nathibitisha taarifa nilizotoa ni sahihi na kweli

Sahihi ya mzazi /mlezi …………………………………………………..........


168